**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE TAMASHA LA UTAMADUNI MWANZA, TAREHE 8 SEPTEMBA, 2021**

*Mheshimiwa Chifu Msagata Fundikira, Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Machifu Tanzania;*

*Mheshimiwa Chifu Aron Mikomangwa, Kiongozi wa Umoja wa Watemi wa Usukuma na Mratibu wa Tamasha hili la Utamaduni;*

*Waheshimiwa Machifu na Watemi wote mliopo;*

*Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;*

*Mheshimiwa Mhandisi Robert Gabriel, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na Wakuu wa Mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa mliopo;*

*Mheshimiwa Dkt. Christine Mndeme, Naibu Katibu Mkuu wa CCM – Tanzania Bara na Viongozi wengine wa Vyama vya Siasa mliopo;*

*Waheshimiwa Wabunge mliopo;*

*Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu, Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo;*

*Waheshimiwa Viongozi wengine wa Serikali mliopo;*

*Waheshimiwa Viongozi wa Dini mliopo;*

*Ndugu Wananchi, Wana-Habari, Mabibi na Mabwana:*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**"HANGAMAGI BATEMI"**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyetujalia uhai na kutuwezesha kukutana hapa. Aidha, naushukuru Uongozi wa Umoja wa Watemi wa Usukuma, Umoja wa Machifu Tanzania, pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kunialika kwenye Tamasha hili la Utamaduni. Ahsanteni sana.

Hii sio mara yangu ya kwanza kushiriki kwenye Tamasha kama hili. Mwaka 2018, nilishiriki kwenye Tamasha la Urithi wa Utamaduni wa Mtanzania lililofanyika Jijini Dodoma kumwakilisha "KILEKANGANO", Hayati Rais Dkt. Magufuli. Na nakumbuka, siku ile Watemi wa Usukuma nami

walinipa jina la KILELAMHINA likimaanisha **"Mama Mlezi wa Wanyonge**".

Vilevile, mwaka 2019, nilishiriki kwenye Tamasha kama hili ambalo lilifanyika sambamba na Tamasha la Nne la Sanaa na Utamaduni la Afrika Mashariki. Hivyo leo ni mara yangu ya tatu. Na nimesikia, mara hii, Watemi wa Usukuma wamenipa jina la HANGAYA likiwa na maana ya **"Nyota Inayong'ara"**. Nawashukuru sana kwa heshima hii kubwa mliyonipa na namwomba Mwenyezi Mungu anisaidie ning'are sio tu mimi peke yangu bali pia niweze kuing'arisha nchi yangu. Na katika hilo, nawashukuru sana Machifu kwa maneno yenu mazuri mliyoyasema ya kunipa moyo katika kuliongoza Taifa letu. *Wabheja sana.*

***Mheshimiwa Waziri;***
***Waheshimiwa Machifu na Watemi;***
***Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema, nanukuu *"Utamaduni ni kiini ama roho ya Taifa lolote. Taifa lisilo na utamaduni ni sawa na mkusanyiko wa watu wasio na roho"*, mwisho wa kunukuu. Usemi huu unaonesha kuwa utamaduni ni jambo muhimu sana katika Taifa. Na hii ni kwa sababu, kwanza, Utamaduni unasaidia kutambulisha Taifa. Mathalan, Lugha ya Kiswahili ni moja ya utamaduni wetu Watanzania unaotutambulisha kama Taifa.

Zaidi ya hapo, utamaduni unasaidia kueleza historia, mila na pamoja na desturi za jamii ama Taifa husika. Vilevile, utamaduni unasaidia kulinda au

kutunza, kuendeleza na kurithisha maadili mema kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Ni kwa kuzingatia hilo, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Viongozi wa Umoja wa Watemi wa Usukuma kwa kuandaa Tamasha hili la Utamaduni kwa niaba ya Umoja wa Machifu Tanzania.

Ni imani yangu kuwa, kupitia Tamasha hili, Watanzania wamejifunza tamaduni, mila na desturi sio tu za Kabila la Wasukuma bali pia Makabila mengine yaliyoshiriki. Zaidi ya hapo, naamini, Tamasha hili litahamasisha Makabila mengine kutangaza tamaduni, mila na desturi zao. Na katika hilo, nitafurahi sana kama Tamasha hili litakuwa linazunguka kwenye Mikoa kila mwaka ili kuwawezesha Watanzania na watu kutoka

nje kujionea tamaduni, mila na desturi mbalimbali za Watanzania. Ni hili, kusema kweli, litakuwa jambo jema sana.

Kama mnavyofahamu, mbali na faida za utamaduni ambazo nimezitaja, kwenye dunia ya sasa, utamaduni ni biashara na pia ni chanzo kikubwa cha mapato. Hii ni kwa sababu utamaduni ni kivutio kikubwa cha utalii. Kwa nchi za wenzetu, hususan za Asia na zile za Mashariki ya Mbali (China, Japan, Thailand, Indonesia), utamaduni ni kivutio kikubwa cha watalii. Hata hapa karibu kwa wenzetu Ethiopia, utamaduni umekuwa kivutio kikubwa cha watalii.

Hivyo basi, sisi nasi hatuna budi kuelekeza nguvu katika kukuza utalii wa kitamaduni. Niliwahi kusikia, kuwa, moja ya mambo yanayofanya nchi yetu ipokee idadi ndogo ya watalii na watalii wengine wanaokuja nchini kutorejea, ni kuwepo kwa wigo mdogo wa utalii. Utaliii wetu umejikita zaidi kwenye maliasili (Wanyama, misitu, fukwe, milima, maporomoko). Na hii pia inachangia watalii wanaokuja nchini kukaa kwa siku chache.

Hii ndiyo sababu Serikali yetu hivi sasa imejipanga kikamilifu katika kuhakikisha inapanua wigo wa vivutio vya utalii, ukiwemo utalii wa utamaduni. Na katika hilo, kama mnavyofahamu, kwa zaidi ya wiki sasa, nilikuwa kwenye Programu ya Kundaa Filamu ya

Kutangaza Fursa na Vivutio mbalimbali vilivyopo nchini. Mojawapo ya vivutio tunavyovitangaza ni utamaduni wetu. Tulianza kule Zanzibar, jana nilikuwa Manyatta (Ngorongoro) kuonesha utamaduni wa Wamasai na leo tupo hapa Mwanza kuonesha utamaduni wa Kabila la Kisukuma. Na zoezi hili ni endelevu. Tunakusudia kutangaza fursa zote za utalii wa utamaduni tulizonazo. Kama mnavyofahamu, nchi yetu ina utajiri mkubwa wa utamaduni kupitia zaidi ya makabila 120 tuliyonayo. Hivyo, tumejipanga kuyahamasisha makabila yote hayo kutangaza tamaduni zao. Na hapa nataka niseme kuwa nimejipanga kuandaa Mashindano yatakayoshindaniwa na Mikoa yote, ambapo mshindi atakabidhiwa Kombe.

***Mheshimiwa Waziri;***

***Waheshimiwa Machifu na Watemi;***
***Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Katika Risala yake, Kiongozi wa Umoja wa Watemi wa Usukuma, kwa niaba ya Umoja wa Machifu Tanzania, amewasilisha baadhi ya maombi na kutaja changamoto zinazowakabili katika kutekeleza shughuli zao za kila siku. Miongoni mwa mambo aliyowasilisha ni ombi la kutambuliwa rasmi Umoja wa Machifu wa Tanzania na kupata Usajili; pamoja na kupatiwa eneo Dodoma ili kuanzisha Ofisi na miradi itakayouwezesha Umoja huo kujiendesha kiuchumi.

Ameeleza pia changamoto ya kupoteza umiliki wa majengo na upatikanaji nyara za Serikali kwa ajili ya kuzitumia kwenye shughuli za kila siku. Changamoto nyingine zinahusu ubovu wa miundombinu kwenye

vituo vya makumbusho; kuvamiwa kwa maeneo ya himaya za jadi na utata wa umiliki wa Kiwanja cha Michezo hapa Kisesa.

*Waheshimiwa Machifu na Watemi,* maombi na changamoto hizi zote ni za msingi na sisi Serikali tumezipokea. Na katika kushughulikia baadhi ya changamoto mlizozieleza, Serikali tayari imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Utamaduni, ambapo kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, tumeupatia bajeti ya **shilingi bilioni 1.5**. Aidha, hivi sasa tupo kwenye mchakato wa kuandaa Sera mpya ya Utamaduni itakayolinda maadili, mila na desturi zetu lakini pia itakayoendana na mazingira ya sasa ya dunia. Lakini niiagize Wizara, katika kuandaa Sera hiyo mpya

ya Utamaduni, wahakikishe wanawashirikisha Machifu na Watemi ili kupata maoni yao. Na katika hilo, mimi binafsi, katika kuendeleza Utaratibu niliojiwekea wa kukutana na makundi mbalimbali, nimejipanga nikutane na Kundi hili muhimu Machifu ili kujadiliana nalo masuala mbalimbali, ikiwemo changamoto zinazowakabili.

***Mheshimiwa Waziri;***
***Waheshimiwa Machifu na Watemi;***
***Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana;***

Tumekutana hapa kwa ajili ya kuhitimisha Tamasha la Utamaduni. Lakini, kabla sijahitimisha hotuba yangu, narudia kusisitiza umuhimu wa kuandaliwa kwa Matamasha kama haya ili kutangaza tamaduni, mila na desturi zetu Watanzania. Aidha,

kupitia kwenu Machifu na Watemi, nawasihi viongozi wa kimila kote nchini kuendelea kusimamia maadili mema kwenye jamii. Zaidi ya hapo, natoa rai kwenu kuendelea kushirikiana na Serikali katika kudumisha amani na usalama nchini, na hasa katika kusuluhisha baadhi ya migogoro inayotokea kwenye jamii zetu.

Sambamba na hilo, kama mnavyofahamu, dunia pamoja na nchi yetu hivi sasa inakabiliwa na changamoto kubwa ya ugonjwa wa *Corona*. Viongozi wa kimila mnao ushawishi mkubwa kwenye jamii. Hivyo basi, nawasihi sana mshirikiane na Serikali katika kuwahimiza Watanzania kuchukua tahadhari zote za kujilinda dhidi ya janga hili lakini pia kutafuta tiba ya kupambana na ugonjwa. Kama tunavyofahamu, sisi

Watanzania tuna tiba nyingi za asili ambazo, naamini tukizifanyia utafiti wa kutosha, upo uwezekano wa kupatikana kwa tiba ya ugonjwa huu pamoja na magonjwa mengine.

Jambo jingine ambalo ningependa kuwaomba Waheshimiwa Machifu na Watemi ni kwamba, mwakani nchi yetu itafanya zoezi la Sensa. Zoezi hilo ni muhimu katika kufahamu idadi ya watu na kupanga mipango na mikakati ya maendeleo. Hivyo basi, kwa kutambua nafasi yenu viongozi wa kimila, nawahimiza kuwahamasisha wananchi kushiriki kwenye zoezi hilo.

*Hangamagi Watemi*, nihitimishe hotuba yangu kwa kurudia kuwashukuru kwa kunialika kwenye Tamasha

hilo. Nawapongeza pia kwa maonesho mbalimbali yaliyofanyika. Kwa namna ya pekee sana, nawashukuru kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa Chifu Mkuu wa Machifu wa Tanzania. Ahsanteni sana.

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru na kuwapongeza Viongozi wa Wizara ya Utamaduni na Mkoa wa Mwanza kwa maandalizi mazuri. Kwa hakika, Tamasha limefana sana. Hongereni sana. Baada ya kusema hayo:

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Mungu Ubariki Utamaduni wa Mtanzania!**

**Mungu Ibariki Tanzania!**

**“AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA”**